**Mr. Stephen Gitagama**
Afisa Mkuu Mtendaji wa Kampuni



# Ripoti Ya Afisa Mkuu Mtendaji Wa Kampuni

Soko la Afrika Mashariki lilikuwa na uhakika wa kukua mwaka 2022, ukuaji ambao ulichangiwa pakubwa na maendeleo katika sekta ya kibinafsi, kurejea kwa shughuli za kawaida katika utoaji wa huduma pamoja na viwanda, kupungua kwa viwango vya maambukizi ya UVIKO-19, umoja wa kikanda na kurejea kwa sehemu ya awali ya uzalishaji katika sekta ya kilimo. Kadhalika, mageuzi ya kidijitali yalichangia katika kuchochea mageuzi ya kiuchumi kwenye ukanda huu kwa kuwezesha uundaji wa nafasi za kazi na uvumbuzi katika tasnia tofauti.

Hata hivyo, chumi za ukanda huu zilishuhudia kudorora kwa mazingira ya uchumi mnamo 2022 kutokana na hali za kifedha kama ilivyoelezewa katika Taarifa ya Mwenyekiti. Mwaka unaoangaziwa NMG ilizindua kampeni na matukio mapya yaliyolenga hali ya matumizi ya watumiaji, mipango ya majaribio ya bidhaa mpya, kutoa maudhui ya aina yake kwenye majukwaa yake yote, kushirikiana na idara zote na kufanya ushirikiano wa kimkakati unaoendesha ajenda ya biashara yetu. Kutokana na hayo, tulishuhudia ukuaji katika mapato kwenye ofisi za kikanda, kufuatia kufunguliwa tena kwa uchumi wa Uganda na kuongezeka kwa viziada pamoja na matukio ya kiubunifu nchini Tanzania. Kadhalika, soko la Kenya liliboresha mipango yake inayozalisha mapato, ikijumuisha ongezeko la mauzo ya tiketi za matukio kupitia *Kenyabuzz.*

### Utendaji wa Kifedha

Faida ya Kampuni kabla ya ushuru ya Shs. bilioni 0.5 ilikuwa kiwango cha chini kuliko mwaka uliopita. Biashara yetu ilipitia changamoto katika mwaka wa 2022 wakati ukanda huu ulikumbana na kiangazi kilichodumu kwa muda mrefu, kupanda kwa gharama za kawi, kudorora kwa viwango vya matumizi ya mtumiaji pamoja na hali tete ya kisiasa. Vigezo hivi vidogo vya kiuchumi vilisababisha kuhujumika kwa mazingira ya biashara, huku kupungua kwa shughuli kukishuhudiwa zaidi nchini Kenya. Utendaji wa jumla ulilindwa kwa kiasi fulani na ukuaji wa mapato kutokana na bidhaa zetu za kipekee- *Business Daily, The EastAfrican na Taifa Leo* na kuongezeka kwa mapato kutokana na bidhaa na huduma za kidijitali na matukio ya hali ya matumizi ya bidhaa.



**Aidha katika mwaka unaoangaziwa NMG ilizindua kampeni na matukio mapya yaliyolenga hali ya matumizi ya watumiaji, mipango ya majaribio ya bidhaa mpya, kutoa maudhui ya aina yake kwenye majukwaa yake yote.**

Hata hivyo, viwango vya faida za Kampuni viliathiriwa pakubwa na ongezeko la ghafla la gharama ya uchapishaji wa habari kote duniani na kudorora kwa thamani ya Shilingi ya Kenya dhidi ya Dola ya Marekani, hali iliyochangia kupanda kwa gharama ya kuagiza malighafi. Kampuni imedumisha ufanisi katika kuthibiti gharama na kuimarisha utendakazi kutokana na mikakati ya kuboresha biashara.

### Shughuli za Utafutaji Soko Kikanda

**Kenya**

Gazeti la *Business Daily* lilisanifiwa upya kwa lengo la kutoa kipaumbele kwa masuala ya kidijitali kwa mkakati uliojaa maudhui ya biashara. Hii ilisababisha bidhaa hiyo kuboreshwa katika uwepo wake kwenye machapisho, majukwaa ya kidijitali na mitandao ya kijamii. Aidha, mnamo 2022, *NTV Kenya* ilifanikiwa kuzindua wavuti wake ulioboreshwa ambao uliiwezesha kutoa maudhui yakutosha ya habari-anuwai kwa muda halisi ili kuwashirikisha watumiaji wa maudhui yake kwa kuwapa habari na taarifa za hivi punde na zinazowafaa zaidi. Huku chapisho la utafiti la Kantar likiashiria kwamba hadhira ya Runinga pia hugeukia intaneti ili kupata habari na taarifa, wavuti huo wa habari-anuwai utaendelea kuwezesha hadhira kufikia maudhui popote walipo.

*Top 40 under 40,* mradi wa *Business Daily* unaolenga kusherehekea viongozi wanaoleta mageuzi na waliopata mafanikio makubwa nchini, mwaka jana ulianzisha *Top40 Club,* ambalo ni jukwaa la mtagusano na ujuzi linalokutana kila robo mwaka na kuleta pamoja waliofuzu katika Top 40 pamoja kwa vipindi vya maarifa na kuwashirikisha. Uzinduzi huo, uliofanywa chini ya kauli mbiu ya, *Uongozi, Lengo na Uendelevu,* ulijumuisha gumzo na Paul Polman, kiongozi na mwanaharakati wa biashara ambaye alikuwa mmoja wa waandishi wa *"Net Positive: how courageous companies thrive by giving more than they take"* kitabu ambacho kilitawazwa kama Kitabu Bora cha Biashara cha Mwaka 2021 na shirika la Financial Times.

*Tuzo za SME za Top 100* zilizinduliwa tena baada ya kusitishwa kwa miaka miwili kutokana na tandavu ya UVIKO-19, huku tuzo za 2022 zikitambua kwamba ni sharti biashara ziwe na ufahamu wa kijamii wa




Kushoto-Kulia: Jeremy Awori, Phyllis Wakiaga na Stephen Gitagama kwenye hafla ya Uzinduzi wa Top 40 Club huko Capital Club

# Ripoti Ya Afisa Mkuu Mtendaji Wa Kampuni (inaendelea)



Kwa makini sana, washindi wanafuatilia programu ya chakula cha jioni (chajio) kwenye hafla ya Top 100 SMEs Gala Dinner nchini Uganda

**Mwaka 2022, tuliwazia na kutekeleza matukio mengi mapya ili kufikia hadhira yetu tofauti ili kutatua mahitaji yao.**

mazingira na jumuiya yao ili kufanikiwa kwa kweli na kuunda thamani kwa ajili yao na washikadau wao. Kutokana na hayo, tulianzisha kategoria mpya ya tuzo ambayo inalenga uendelevu, Kuwajibika kwa Kampuni Kijamii (CSR), uanuwai na ujumuishaji. NMG imewekeza katika kuhakikisha kwamba mbali na tuzo hizo, Biashara Ndogo na za Wastani (SMEs) zina uwezo wa kufikia taarifa, fursa za kujifunza kutokana na safari na mawanda ya wajasiriamali wengine kupitia kwa machapisho na matukio yetu mengine kama vile *Kongamano la SME na Maonyesho* miongoni mwa mengine.

Mwaka 2022, tuliwazia na kutekeleza matukio mengi mapya ili kufikia hadhira yetu tofauti ili kutatua mahitaji yao. Tulianzisha *Mancave*, tukio la kutangamana kwa ajili ya wanaume pekee. Tukio la kwanza lilivutia mamia ya wanaume na likaweka msingi kwa tukio hilo kuwa msururu mwaka 2023. Kadhalika, tuliandaa *Chajio Kuu cha Siku ya Kimataifa ya Wanawake,* tukio lililotoa nafasi ya kusherehekea wanawake na kupigania usawa wa kijinsia. Katika robo ya mwisho ya mwaka, tulianzisha *Mental Wellness and Counselling Breakfast,* tukio ambalo lilileta pamoja washikadau wa HR na waajiri ili kujadili suala la afya ya kiakili na jinsi inavyoathiri watu katika sehemu za kazi na mipango ya kuweka mazingira salama ya kufanyia kazi.

Katika robo hiyo hiyo ya mwaka, tulifanya *Job Fair and Conference,* tukio lililoandaliwa kwa ushirikiano na Huawei lililoleta pamoja watu wanaoweza kuwa waajiri na watu wanaotafuta kazi ili kujadili changamoto katika ajira nchini Kenya, fursa kwa watu waliofuzu majuzi, na ushirikiano wa kupanua mawanda, miongoni mwa mengine. Tukio hilo lilivutia maelfu ya watu wanaotafuta kazi, mamia ya waajiri na lilihudhuriwa na Naibu wa Rais wa Jamhuri ya Kenya, Mheshimiwa Rigathi Gachagua na maafisa wengine wa serikali.

### Monitor Publications Limited (MPL) @ 30

MPL nchini Uganda ilisherehekea miaka 30 ya kuwepo mnamo mwaka 2022. Katika wakati huu, iliendelea kushuhudia ukuaji wa Uganda na kuendesha msingi mkuu wa kuwepo kwa NMG - kuwa sauti kwa wanyonge, ajenda ambayo imepigania kwa miaka mingi.

Gazeti la *Daily Monitor,* ambalo inachapisha, limekuwa likifanya vyema katika soko la Uganda kwa miaka mingi, lilikuwa la kwanza kuchapishwa kwa rangi kamili nchini humo, limekuwa ni uwanja wa mafunzo kwa wanahabari, limepigania uhuru wa wanahabari na linajivunia wavuti mkubwa zaidi wa habari katika nchi hiyo nzima.

Gazeti hilo la Uganda lilisherehekea maadhimisho mwaka huu, chini ya kauli mbiu ya *"Kusherehekea ya Zamani na Kutoa Taswira ya Siku za Baadaye"* katika halfa ya kiamsha kinywa na mkutano wa hadhara katika Hoteli ya Serena na kualika washikadau wakuu kutoka kote nchini. Liliendelea kufanya mipango yake mbalimbali kuanzia zahanati zake za aina yake za mashamba, *Rising Woman Initiative, Top 100 Medium Sized* Companies na kuzindua matoleo mawili mapya ya gazeti– matoleo ya Tesa na Luka Kalangala.

### Mwananchi Communications Limited (MCL)

MCL iliandaa awamu ya pili ya *The Citizen Rising Woman Initiative* chini ya kaulimbiu ya *"Usawazishaji leo kwa kesho endelevu"*. Mpango huo unalenga kukuza uwezo wa viongozi wanawake wa kuchukua nafasi za uongozi katika asasi za umma na za kibinafsi na kuchangia katika ukuaji wa biashara katika ulimwengu shindani unaobadilika. Kabla ya hii, MCL iliandaa *The Citizen Women in Energy Breakfast* kama tukio la kutangulia lile la *The Citizen Rising Woman.* Tukio hilo lililenga kutambua na kusherehekea watu wanaofanya zaidi ya mwito kwao kuwezesha na kukiri nafasi ya mwanamke katika sekta ya kawi.

Kadhalika, mwaka huo ulishuhudia ushirikiano wa MCL na *Vodacom Tanzania* kuzindua *eGazeti* kwenye Programu ya My Vodacom ili kuwapa wasomaji uwezo wa kufikia magazeti ya *Mwananchi, Mwanaspoti* na *The Citizen* kwa urahisi mtandaoni.

# **Ripoti Ya Afisa Mkuu Mtendaji Wa Kampuni** (inaendelea)




**Wanajopo wajadili kuhusu mbinu za kubadilisha na kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi katika kongamano la masuala ya tabianchi huko Kampala, Uganda**

Kampeni ya *"Habari Ziendelee"* ilizinduliwa kwa lengo la kutoa uhamasisho kuhusu ushirikiano na kukuza idadi ya wasomaji. Katika mwaka huo mzima, shirika hilo liliendesha maonyesho ya zahanati za mashambani, mipango ya *Mwananchi Thought Leadership Forum na Newspapers in Education (NiE)*, ikisababisha ushirikiano mpya na sekta za umma na za kibinafsi ili kuongeza viwango vya shughuli na kuleta athari nchini.

### Safari ya Mazingira, Jamii na Uongozi (ESG)

Katika mazingira ya sasa, biashara endelevu, athari ya kijamii, shabaha, ushirikishaji wa jamii na maadili ya pamoja ni maneno ambayo yananasibishwa na jumuiya ya biashara kote duniani. Aidha, tandavu ya UVIKO-19 iliongeza hitaji la uongozi wa mashirika kusawazisha mahitaji ya shirika, ya kimazingira, kijamii na binadamu na masuala kama vile mabadiliko ya tabianchi, usawa wa kijinsia, afya ya kiakili na mengine yanayoibuka.

Katika enzi ambapo watumiaji wanakumbatia chapa na biashara zenye shabaha zinazoleta thamani kwa washikadau wake na jamii, imekuwa muhimu kujumlisha uendelevu katika operesheni zetu. Hii inamaanisha kusawazisha mahitaji ya Kampuni ya sasa na mahitaji ya vizazi vijavyo.

Katika ripoti inayojadili umuhimu wa kuripoti masuala ya Mazingira, Jamii na Uongozi (ESG), KPMG iliashiria kwamba ESG ni muhimu katika mkakati wa kampuni hiyo, na kwamba kampuni

**Safari ya ESG itatuwezesha kufanya hili haswa, kuchunguza athari yetu kwa jamii kwenye vigezo vya kimazingira, kijamii na uongozi na kufanya maamuzi ya muda mrefu na mikakati ambayo inasababisha masilahi bora ya washikadau wetu**

zinaweza tu kufaulu baada ya muda mrefu ikiwa zinalinda watu walio katika msururu wao wa usambazaji, wateja, wafanyakazi na mazingira yao. Si kitendo cha ubinafsi—ni biashara na ni muhimu pande zote zifaidike.

NMG inapofanya safari yake ya kutaka kuwa shirika shupavu, linalolenga wateja na linaloendeshwa na data, uendelevu utakuwa kigezo muhimu kinachowezesha kuendesha uendelevu wa biashara kwa kuleta manufaa ya kudumu kwa jamii. Lengo ni kuendelea kudumisha Kampuni hiyo kama chaguo la kimkakati na la kudumu la mshirika.

Safari ya ESG itatuwezesha kufanya hili haswa, kuchunguza athari yetu kwa jamii kwenye vigezo vya kimazingira, kijamii na uongozi na kufanya maamuzi ya muda mrefu na mikakati ambayo inasababisha masilahi bora ya washikadau wetu mbalimbali na Kampuni. Kufuatia tathmini yetu ya awali, tumetambua masuala mbalimbali ya msingi ambayo tutaendelea kufuatilia na kuripoti kuhusu. Haya yanaanzisha uanahabari wa kuwajibika, uongozi wa kampuni, athari ya kimazingira, ustawi wa wafanyakazi na athari ya kijamii, ambayo yatashughulikiwa kwenye ripoti hii.

Tunatambua kwamba tunaweza kuwa katika hatua za mwanzo za safari hii katika kuunda mfumo, kutambua vipengele vyetu muhimu na kuweka mikakati na hatua kwa nyanja zetu za athari kubwa, lakini tumejitolea kuenda masafa hayo na kuleta athari.

### Utambuzi wa Kimataifa

*Tuzo za Kusi Ideas Festival* zilitolewa kwa mwaka wa pili mfululizo katika Tuzo za Kimataifa za Shirikisho la Vyombo vya Habari vya Kimataifa mwaka 2022, tukichukua nafasi ya kwanza katika kategoria ya *"Best Use of an Event to Build a News Brand"* huku *Nation.Africa* ikipata kutajwa kwa taadhima katika kategoria ya Mpango Bora wa Kupata Watumiaji Wanaojisajili. Nchini Tanzania, MCL ilikuwa ya kwanza katika Tuzo za Mwajiri Bora wa Mwaka katika kategoria ya Usawa na Usawazishaji wa Kijinsia, na kushinda kitengo cha Ufanisi katika Mauzo ya Tukio katika Tuzo za Sayansi ya Mauzo za Tanzania. Wafanyakazi wa NMG kutoka kote katika ukanda huu walituzwa na taasisi mbalimbali – wafanyakazi 18 walitambuliwa nchini Tanzania, 14 nchini Uganda na 31 nchini Kenya.

### Mageuzi ya Shirika

Kwa miaka sasa, tasnia ya habari kote duniani imepitia changamoto, zilizolazimu mashirika kutathmini upya mikakati na uwezo wao wa kuhakikisha kwamba yanakuzwa vyema ili yawe tayari kwa lengo na yawe mashirika endelevu yanayozungumza lugha ya watumiaji. Kwa hivyo Kampuni hii inageuzwa kuwa shirika shupavu, linalolenga wateja na linaloendeshwa na data ili kuwapa thamani wateja, wafanyakazi na wenyehisa.

NMG inaendelea kufanya mageuzi ili kutuwezesha kuangazia zaidi vigezo

# Ripoti Ya Afisa Mkuu Mtendaji Wa Kampuni (inaendelea)



Washiriki wanapanga foleni ya maombi ya kazi na ushauri kuhusu taaluma katika hafla ya Nation Huawei Job Fair kwenye ukumbi wa KICC

> **Tunapopiga hatua za kufanyia mabadiliko njia yetu ya kufanya kazi kwa ajili ya siku za baadaye, tunaendelea kupata fursa za kuboresha biashara yetu ya sasa, kuanzia uchapishaji hadi utangazaji hewani.**

vikuu vinavyotuwezesha kufanya uundaji huu wa thamani utimie. Tutawekeza katika utafiti wa kina ili kujua na kuelewa hadhira yetu na kuunda bidhaa wanazozipenda kwa kutumia mbinu inayoendeshwa na majaribio, uundaji wa bidhaa kwa kuenda sokoni, mbinu ambayo itatuwezesha kufanyia maudhui, bidhaa au huduma zetu majaribio kabla ya kuzindua sokoni kikamilifu.

Mbinu hii itatuwezesha kuwekeza katika teknolojia inayofaa na kuunda upya bidhaa zetu, kuzifanya ziwe za kufaa hadhira yetu iliyopo na hadhira mpya na kuunda programu ambazo zitatumika kama viendelezi vya ofa zetu zilizopo za kushirikisha wateja, kuhimiza usomaji nje ya mtandao na kuandikisha hadhira mpya.

Ili kutuwezesha kufanikisha haya, tunaendelea kuweka pamoja kanikazi ya siku zijazo kwa kuimarisha uwezo katika shirika na katika masoko tofauti. Tunatambua mianya iliyopo kati ya ujuzi unaohitajika kwa ajili ya kupangia mustakabali ikilinganishwa na seti ya ujuzi wa wafanyakazi tulio nao kwa sasa na kuwekeza kwao kwa nia ya kuhakikisha kwamba ndio bora katika majukumu yao husika, kuanzia uhandisi hadi uundaji wa bidhaa na dijitali, miongoni mwa mengine. Utafiti na tathmini za awali zimeashiria kwamba asilimia ndogo ya maudhui yetu ndio inaleta ushiriki wa juu zaidi kutoka kwa hadhira zetu. Kutokana na hayo, tunaboresha ujuzi wa wanahabari wetu kwa nia ya kuunda maudhui ya ubora wa juu na ya media anuwai.

Tunapopiga hatua za kufanyia mabadiliko njia yetu ya kufanya kazi kwa ajili ya siku za baadaye, tunaendelea kupata fursa za kuboresha biashara yetu ya sasa, kuanzia uchapishaji hadi utangazaji hewani. Ripoti ya Hali ya Vyombo vya Habari ya 2022 iliyotolewa na Baraza la Vyombo vya Habari la Kenya (MCK) iliashiria kwamba Televisheni na redio zinaongoza kama majukwaa yanayotumiwa na Wakenya kupata habari. Kutokana na hayo, tunaamini kwamba kuna uwezo mkubwa katika biashara yetu ya utangazaji hewani kote katika ukanda huu na tutaendelea kuwekeza huko ili kuvuna fursa zake za ukuaji.

### Shukrani

Ninashukuru kwa dhati wateja wetu ambao walisoma, kutazama au kusikiliza maudhui tunayozalisha na wale wanaoamini bidhaa zetu kupeperusha ujumbe, kampeni na mafanikio yao. Kwa sababu yenu, tunaendelea kuvumbua na kuwahudumia vyema zaidi.

Kwa wafanyakazi wa Kampuni walio nchini Kenya, Tanzania, Uganda na Rwanda, Ninasema asante sana, kwa ustahimilivu, kujitolea, ari na uthabiti mlio nao – sifa hizi zimekuwa nguzo ya kuendesha biashara mbele katika tasnia ambayo imekumbwa na changamoto katika mwaka uliopita.

Kwa Bodi yetu ya Wakurugenzi, washirika na wenyehisa wetu, mnaendelea kutuamini na kutoa usaidizi usio na kifani kwa yale tunayoyafanya, na kwa sababu hiyo, tunawashukuru.

Tunapotazamia mwaka mpya, ninaamini tunaingia katika enzi mpya ya biashara, ambapo tunaleta thamani kwa washikadau wetu zaidi ya kitu chochote kingine. Ninatazamia kuendelea kushirikiana nanyi ili kufanikisha haya.

**Stephen Gitagama**
Afisa Mkuu Mtendaji wa Kampuni

A BIRD'S EYE-VIEW OF ACQUISITIONS AND MERGERS. IN-DEPTH REVIEWS OF TECHNOLOGY AND INNOVATION. FROM THE STOCK EXCHANGE TO LIVESTOCK FARMING, WE ARE THE BOND BETWEEN NOW AND TOMORROW.

24 insightful pages of comprehensive business news, features, lifestyle segments, technology and so much more.

→ #MorePossibilities

BD
Business Daily

Grab your copy or join us online
*everyday to keep informed.*